Baada ya taarifa fupi ilifuatia (feedback) mrejesho wa tathmini ya siku ya kwanza iliyotolewa na Dr. Christopher kuhusu Evaluation ya wanawarsha ya day one, baada ya hapo kipindi cha kwanza kilianza na mwezeshaji Mwinjilisti Kimani. Mada kuu ilikuwa ni MAWASILIANO – alifundisha maana ya mawasiliano kuwa ni dhana inayohusisha mtoa ujumbe na mpokea ujumbe akatukumbusha pia kuhusu team work watu muhimu wa kushirikiana ni Afisa Mtendaji wa Kijiji, Balozi, na Mwenyekiti, ni watu muhimu kwa mawasiliano kuhusu mgonjwa pia akawa ametueleza aina za mawasiliano. Vipengele vya mawasiliano, vikwazo vya mawasiliano, vitendo vinavyoonyesha kujali mawasiliano, vitendo vya kutokujali mawasiliano, umuhimu wa mawasiliano bora, faida za mawasiliano bora, stadi (mbinu) bora za mawasiliano, masuala muhimu ya kuzungumzia kama vile dawa, chakula na mazingira ya hapo anakoishi mgonjwa. Pia mambo muhimu ya kukumbuka wakati wa mawasiliano kama vile jinsi ya kutoa ujumbe, ni ujumbe gani unatakiwa kutolewa na ni wakati gani n.k. Baada ya hapo Mwenyekiti alikaribisha wanawarsha kuuliza maswali kuhusu mada ya mawasiliano, wanawarsha walichangia vizuri, na Mwenyekiti Mch. Safari alisummarize jinsi ya kumweleza mgonjwa ukweli kuhusu tatizo lake, kwanza kabisa tumwandae mgonjwa tumwulize mgonjwa kama yupo tayari kujua tatizo lake au hayupo tayari. Usimwambie mpaka siku atakayokuwa tayari, mtoa mada alipongezwa. Mgonjwa awezeshwe kujua na kueleza tatizo lake mwenyewe.

Kipindi cha kupata chochote kilifuata yaani (tea time). Baada ya kipindi cha chai nzito ya maziwa iliyosindikizwa na rafiki yake kababu, donati na matango kwa wingi wanawarsha pamoja na wawezeshaji walikuja na nguvu mpya ya kumsikiliza baba yetu Mch. Kimerei. Mchungaji alianza na neno la kukazia kuwa Mwinjilisti na Dr. ni watu wanaotegemeana haina haja ya mmojawapo kumdharau mwingine, wanahitaji kushirikiana ili kukamilisha kazi ya uponyaji kimwili na kiroho, pia alituonyesha dawa na akasema maana yake, ikifuatiwa na msalaba, na picha ya mikono miwili iliyoshikana na kutueleza maana yake. MADA KUU ya somo alilotoa Mch. Kimerei ilikuwa ni Spirital Care mwezeshaji alieleza maana ya HOSPICE kuwa ni faraja, ukarimu unaotolewa kwa wale wanaostahili kukirimiwa na maana hii iling'arishwa na maandiko matakatifu toka Luka 6:36 "Iweni na huruma kama baba yenu alivyo na huruma,"

alikazia kuwa watoa huduma hii ya Palliative Care washike sehemu anapoumwa mgonjwa ili afarijike. Pia mgonjwa anatakiwa aheshimiwe, kinyume na hapo unamnyanyapaa mgonjwa.
Pia Mchungaji alikazia kuhusu hospitali zetu za Kanisa kila mahali tunapotoa huduma kama vile kwenye dawa, sindano, operation (upasuaji) Jina la Yesu litumike kwa wahudumu kuwaambia wagonjwa ili mtu apone, akatolea mfano wa mtu aliyepewa dawa hospitalini hazikubarikiwa akapitisha kwa mganga wa kienyeji zibarikiwe. Pia mwezeshaji alishauri kuhusu mazingira ya hospitali zetu yaweje. Langoni bawabu na mapokezi ni mahali muhimu sana panatakiwa patengenezwe na kuvutia kwa wateja wetu. Kama maneno ya Mungu yalivyosema Mwanzo 28:16, mgonjwa aseme hakika hapa ni mahali penye Mungu hapo atakuwa na nafuu, bawabu na mtu wa mapokezi wawe kivutio: wasafi, wachangamfu pamoja na sala, isiwe kikwazo kwa wagonjwa, pia alisisitiza vitu (watu/wateja) wetu wanavyotazamia kuona kwa wahudumu, kuwa ni watu wanaomcha Mungu wamwone uso kwa uso kusimama pembeni, ili aone kama wanamjali, siyo kama nabii Elisha alivyofanya kwa Naamani Wafalme 5:1-12.

Pia alisisitiza kumshirikisha mgonjwa kwenye mambo ya kiroho alitoa mfano wa mgonjwa alienda hospitali fulani na hirizi sehemu nyingi za mwili wake Dr. alizikuta na kuzitupa, kuwa si kitendo kizuri kudharau imani ya mtu mwingine bora umshirikishe kama akikubali kubadili imani yake ni vema. Na mwezeshaji wetu aliendelea kutupa mifano mingi kuhusu imani za watu mbalimbali ukiwemo mfano wa watu wawili waliogombania shamba, na mtoto na baba yake kisa baba alichinja mbuzi wa mtoto bila ridhaa ya mtoto, na mtoto hakuonyesha utii kwa babaye kapatwa na balaa. Hivyo ilitufundisha dhahiri jinsi watu walivyo na imani zao na zinastahili kuheshimiwa na pia alitueleza aina ya matamshi yaliyotiwa nguvu kama vile tamshi la LAANA na tamshi la baraka. Mtu anayelaaniwa ni mtenda maovu na anayebarikiwa ni Mtenda Mema. Hesabu 6:22-26. Kipindi hicho cha Mch. Kimerei kiliishia saa 12:30pm. Na kilifuatiwa na kipindi cha maswali na majibu. Wanawarsha na wawezeshaji walichangia mawazo na kuweza kujibu maswali na kufikia muafaka, kama vile mjadala wa mgonjwa kuguswa pendekezo ilikuwa ni mgonjwa aandaliwe na kuhusisha jamii kama wapo pale na pia uangalie mazingira ya pale kuwa yanaruhusu mgonjwa kufanyiwa hivyo.

Baada ya mjadala huo kwisha Mwenyekiti aliwakaribisha wanawarsha wawili waliokuwa wamechelewa toka Hospitali ya Nkoaranga wajitambulishe na walieleza wanafanya nini kuhusu Palliative Care hospitalini kwao na walifanya hivyo, na baada ya utambulisho Mwenyekiti alimkaribisha Bwana Sikio kueleza aliyoona day one na alifanya hivyo. Baada ya hapo Facilitator Dr. Christopher na Paulina Natema, Wachungaji/Wainjilisti. Mch. Kimerei na Mwinjilisti Kimani.

Baada ya Heavy lunch wanawarsha walikaa vikundi vyao kama walivyoelekezwa na mtoa mada Dr. Christopher majadiliano yalianza kama kawaida group la Waganga/Nurses walimchagua Katibu wao Epiphania Michael, na mada kuu ilikuwa kuhusu matumizi ya dawa za maumivu kwa wagonjwa wa chronic illness (magonjwa sugu). Mtoa mada alieleza kwa kipindi hiki Morphine hakuna hatuwezi kuacha kufanya Palliative Care, alituelimisha pia kuhusu aina ya maumivu yasiyoisha – Cancer, maumivu mara kwa mara (maumivu kwa kipindi) HIV/AIDS, maumivu ya kawaida kama kuumia,

maumivu ya mishipa – mkanda wa jeshi (herper zooster) na kuna stage tatu za dawa 1st Stage ASA, PCM, Brufen, Diclofenac, Indocid. 2nd Stage Cordenin, Tramadol. 3rd Stage Pethedine na kuelezea kuhusu dose na muda wa kutoa hizo dawa, pia madhara yake na dawa ya kuongezea kama ingine ikishindwa kuondoa maumivu. Na alisisitiza kutokuacha kumpa dawa za maumivu mpaka mgonjwa afe, kutokuogopa kutibu kwa muda mrefu, kuwa shujaa kwani elimu prescriber tunayo na kumweleza mgonjwa inavyotakiwa, kutumiwa na haraka ya kumbadilishia mgonjwa dawa. Tusisahau njia zingine za kumsaidia mgonjwa kupunguza maumivu kama team work baada ya hapo kipindi cha maswali na majibu mazuri yalitolewa na watoa mada wetu Dr. Christopher na P. Natema. Kipindi kiliishia saa 3:30 pm.

Kipindi kingine kilifuata cha HIVI/AIDS PALLIATIVE CARE lugha ya serikali continuum of care – Huduma endelevu, huduma hii haijali mipaka, Antibiotics inayotumika kwa wagonjwa wa HIV/AIDS ni Septrine 2x2, ambao hawapatani watumie Dapsone tabs, pia tulikumbushwa tunapoenda Home Based Care tuende na ORS packets, Amitrypline & Matuts inasaidia (HIV/AIDS pts) pia kuunda vikundi makanisani, jamii na hospitalini vya kuelimisha kuhusu HIV/AIDS.

Vikundi vyote viwili viliingia darasani na kuanza presentation zao kilianza kikundi cha Wainjilisti/Wachungaji waliwakilishwa na Katibu wao Mch. Temu, walitoa Summary yao kuhusu mada walizojadili kama ifuatavyo. Dhana ya matibabu, sura nzima ya hospitali na huduma zote atakazopewa mgonjwa ziwakilishe jina la Yesu, na ajira ya wafanyakazi kwenye hospitali zetu iangaliwe vizuri, habari ya kugusa mgonjwa, na mapendekezo yao kuwa na vikao vya Chaplain, au semina za mara kwa mara waliomba kwa mwezeshaji Dr. Christopher kufanya hivyo. Baada ya hapo tulisikia taarifa ya mada za Wauguzi na DRS toka kwa Katibu Epiphania kama nilivyoeleza hapo juu. Baada ya hapo tulipewa evaluation form za day two na mnamo saa 4:30 kipindi kilifungwa na Mwenyekiti kwa kuwashukuru wanawarsha na watoa mada kwa ushirikiano, na ilifuatiwa na sala fupi toka Mwinjilisti Heriely Mbwambo.

Imetayarishwa na kusomwa na NEEMA ALUTE.

SEMINAR: PALLIATIVE CARE

MADA: MATUMIZI YA DAWA MAHALI PASIPO NA DAWA NZITO: DR. CHRISTOPHER AT AL

Lengo la kutumia dawa ni maumivu (PAIN). Maumivu haya hayajalishi ni ya aina gani ila ni kujua kitu gani kinamsaidia mteja wetu kutuliza maumivu, japo kuna watu wachache ambao wameugua kwa muda mrefu lakini hawana maumivu yoyote.

Ushirikiano wa Mganga, Muuguzi, Mshauri Nasaha, Mchungaji, Mwinjilisti na Jamii utaweza kumsaidia mteja kutuliza maumivu yake.

- Sisi kama Waganga mchango wetu ni upi katika kutuliza maumivu kwa kuwa MORPHINE bado ni tatizo katika kutuliza maumivu kutokana na upatikanaji wake kuwa mgumu karibu 0%.

- Kwa hiyo Msingi mzuri katika kutuliza maumivu ni huduma ya kiroho kama Wakristo.

AINA ZA MAUMIVU

(a) MAUMIVU YA KIPINDI

Maumivu yanakuwepo kwa kipindi kifupi lakini yanajirudiarudia mfano: Waathirika wa UKIMWI walio na maumivu kutokana na kuathirika kwa mishipa ya fahamu kama H.Zosters (Mkanda wa Jeshi).

(b) MAUMIVU YA KUDUMU

Maumivu hayaishi mfano wagonjwa wa CANCER.

DAWA ZA MAUMIVU

Dawa za maumivu zilizokubalika na kuwekewa utaratibu na Shirika la Afya Ulimwenguni WHO ni kama ifuatavyo:-

STAGE I: ASA, PCM, Brufen, Diclofenac, Indocid (NSAD'S).

STAGE II: Codein, Tramadol – kwa maumivu ya kawaida na zinapatikana. Pethedine – inafanya kazi kwa muda mfupi na ina madhara mengi.

STAGE III: MORPHINE – ina bei rahisi lakini sera ya serikali ni kikwazo.

Inj. Diclofenac
Amitryptilline

Protocol ya Maumivu

1. Paracetamol – 2x4 – kwa muda usiojulikana
2. NSAD'S
3. Analgesics + Amitryptilin ½ - 1 Tab kwa siku (usiku).

KUMBUKA

- Usiache kutibu maumivu mpaka mgonjwa afe.
- Usiogope kutibu maumivu kwa muda mrefu bali uogope maumivu yasiyotibika.
- Tuwe na ushujaa katika kuandika dawa kwa kuwa tuna elimu na tunafahamu matumizi yake.
- Usiwe na haraka kutafuta inayomsaidia mgonjwa wako kutuliza maumivu ili kujua kama inamfaa au la.
- Tumia wasaa – hasa mgonjwa anapokuwa wodini ni rahisi kutambua maumivu ya mgonjwa na hatua ya maumivu.
- Tusisahau kuongeza nguvu za dawa (dose).

HUDUMA ENDELEVU KWA WAATHIRIKA WA UKIMWI

- Ni muhimu kutembea na dawa katika kuwatembelea nyumbani. Angalau za maumivu pia antibiotics Mfano: Cotrinoxale – kama zinamdhuru tumia DAPSON.
- ORS
- M/Vitamin
- Kujenga jamii kwa ajili ya kumsaidia mwathirika mfano kuunda vikundi vya waathirika wanaoishi na VIRUSI.
- Tusipotumia Team work hatutaweza kufanikiwa.

Treating Pain Without Morphine
17 February 2005

1. Know the Pain you are treating
   - Constant; if it is this kind of pain, do not ever stop the pain treatment!
   - Intermittent (as in AIDS cases)
   - Visceral/Somatic (usual pain)
   - Neuropathic

2. Know the drugs you are using, beginning with Step 1 drugs from the Analgesic Ladder:
   - Paracetamol: 4 to 6 hours duration, maximum 4 grams/24 hours. Typical long-term dose would be: 2 tabs 4 times daily
   - Aspirin: also 4 to 6 hours duration. Not as well tolerated as PCM but some people tolerate very well. Same long term dose as PCM: 2 tabs 4 times daily
   - Diclofenic: 8 hours or so. Long-term dose is 1 tab 3 times daily. Not as well-tolerated as PCM, and is more expensive, but works better for some kinds of pain
   - Ibuprofen: 6 hours or so. Long-term dose is 2 tabs 4 times daily.
   - Other NSAIDS: if one does not work well, try another one. But usually pain which is not responsive is asking for a higher potency of drug. Side-effects of all of these drugs except PCM (which is the best tolerated of all) are the same: GI upset is the main one. Kidney damage is the next serious potential side effect.

3. Step 2 drugs from the Analgesic Ladder:
   - Codeine: if it is available, one half tablet 4 times daily is a good starter dose. If no good response in 48 hours, go to one whole tablet 4 times daily. Sedation and constipation are the predictable side-effects.
   - Tramadol: one tab 4 times daily is the usual dose. Side-effects are like codeine: GI upset, constipation, and sedation
   - The main problem with these Step 2 drugs is that they are too expensive, more than 300 shillings per tablet.

4. Step 3 drugs from the Analgesic Ladder:
   - Pethidine: this drug only lasts 3 to 4 hours by injection. It is a terrible drug for constant pain because after 48 hours many people get CNS side effects such as confusion and agitation.
   - Diclofenic injection: lasts for up to 8 hours and is therefore a better hospital drug than pethidine. But it is much LESS potent when given orally. Then it is only a Step 1 drug.
   - Oral Morphine: hopefully this drug will become available to your institution. It is inexpensive, easy to use, and very effective. There is no need for codeine or tramadol is oral morphine is available.

5. Consider adding Amitryptaline to tough pain cases:
   - Amitryptaline is helpful with "neuropathic pain". It will not help ordinary pain, BUT consider other effects of this drug: it helps with sleep; it helps with appetite; it may help with depression.
   - Dose is one half tab (a usual tab is 25 mg) at bedtime, in combination with any one of the Analgesic Ladder drugs such as PCM or Ibuprofen. This can be increased to a whole tab at bedtime after one week if no good effect.
   - Advantage of this drug: it is very inexpensive and very available
   - Disadvantages: none. If it is not helpful, the client can stop it after some time.

6. Protocol for pain without morphine:
   - PCM routinely. If effective, this is the safest long-term drug
   - If PCM ineffective, try an NSAID i.e. Ibuprofen or Diclofenic.
   - If the first NSAID does not work, try one more
   - If still ineffective, add low dose amitryptaline (half tab). Use it in combination with whatever Step 1 drug was best tolerated.
   - If still ineffective, make amitryptaline a whole tab.
   - If still ineffective, look for funds to help with Tramadol.

Remember:
   - Do not stop treating pain unless you think the pain is gone
   - Some pains last for years i.e. cervical cancer
   - Because you spend more time listening to clients and trying to understand their pain, you will know more about their treatment than most prescribers. Be confident!
   - Finding the right combination of pain drugs for a person can take time, but should not take more than 2 weeks.
   - This approach can be used on the hospital wards the same as in the home. Evaluate DAILY if the pain is very severe.
   - Many pains have a spiritual and psychological component which MUST be addressed in order for the medicines to be effective.

KAZI YA KIKUNDI (WATUMISHI WA KANISA)

UTANGULIZI

Huduma za kiroho hospitalini zifufuliwe ama zirudi katika hali yake kama Bwana Yesu alivyoagiza.

Tunapotazama maana ya “Hospice” na “Palliative Care” kwamba ni huduma ya faraja na ukarimu kwa wagonjwa wenye magonjwa ya kusendeka majumbani, hospitalini na mahali popote walipo.

∴ Hivyo basi kwa njia zisizokuwa rasmi kila kabila lilikuwa na huduma hii na makabila mengine yanaendeleza huduma hii.

1. AJIRA NDANI YA HOSPITALI ZETU

Kanisa lijichunguze katika muundo wake, maadili yameporomoka, watu wanajali pesa na kujaza nafasi za kazi zilizo wazi bila kufuata maadili ya Kanisa Mf. kuajiri Waislamu. Watumishi wasio na maadili ya Kanisa n.k. hivyo Kanisa lijirudi/lirudi kwenye nafasi yake.

2. KUGUSA

(a) Baada ya mjadala wa kina, jambo la hekima limesisitizwa sana katika kumhudumia mgonjwa kulingana na mazingira yaliyopo (2Kor: 3).

(b) Kwa wale watumishi wa hospitali (Wachungaji na Wainjilisti) ni vema wakapata elimu ya utunzaji wa wagonjwa ki-uchungaji. Aidha watumishi wajiamini.

(c) Tamko litolewe na uongozi wa juu kwamba kwenye muundo wa utawala hospitalini nafasi ya Chaplain ionekane wazi na itambulike katika umuhimu wake.

(d) Chaplains watambue wajibu wao.

(e) Kuwa na vikao vya mara kwa mara kati ya Chaplain na wakuu wa idara ndani ya hospitali kuhusu kutoa huduma katika misingi ya kiroho mf. Nakupa dawa hizi katika Jina la Yesu chukua na ukatumie.

(f) Ziwepo tracks mbalimbali zenye ujumbe wa Neno la Mungu Hospitalini.

(g) **UKIMWI**

Baada ya mjadala wa kina wajumbe wamependekeza kwamba ni vema ikawepo ridhaa ya mgonjwa juu ya kutambulika ugonjwa wake. Mf. wanandoa kama ni mume au mke ameathirika iwepo ridhaa ya mmoja katika kumfahamisha mwingine na sio mshauri kuwa msemaji wa

mwisho. Ushauri wa jumla na wa kina ufanyike kwa kuzingatia misingi ya washauri nasaha.

3. KUONGEA KICHUNGAJI

Mashauri yote ya kiroho yamhusuyo mgonjwa ni vema yakafanyika mazingira ya hospitali ili kukwepa kutoa mwanya kwa mgonjwa kwenda kutafuta hayo kwa waganga wa kienyeji au kwenye imani nyingine zinazozuka siku hadi siku.

4. UHUSIANO

Madaktari na Chaplains wazingatie sana jambo hili ili huduma hii iende kama Yesu alivyoagiza.

Pendekezo

1. Haki za machaplain zifahamike na wapewe kipaumbele katika hizo:-

   (i) Kwenda shule ili …… ndani ya wakati uliopo katika mazingira yake.

   (ii) Umoja wa Chaplains udumishwe ndani ya ELCT.

   (iii) Chaplains wajue majukumu yao na kuyasimamia.

   (iv) Kwa wale wachungaji ambao wanahudumia vituo na sharika ni vema waka-delegate power kwa wengine mf. Wainjilisti, Wazee wa Kanisa au Mkristo mwaminifu atoe huduma kwa mgonjwa badala yake.

   (v) Viwepo vipaza sauti au namna yeyote ile ya kufikisha ujumbe mawodini. Vifaa hivyo si ghali sana na vinapatikana nchini.

OMBI

Tunamuomba Dr. Christopher tuwe na semina za mara kwa mara kama hizi.

MWISHO

Tunatoa neno la shukrani kwa kila aliyehusika katika kutuandalia semina hii. Aidha katika jitihada hizo hizo tunatoa neno la pole kwa wote waliohusika katika shughuli mbalimbali mpaka hapa tulipofikia.

Mungu awabariki sana.

Pastors/Evangelists and HBC

You are not the primary providers of medical care. But
You are part of the team providing medical care i.e. Palliative Care.

In addition to excellent spiritual counseling and being willing to visit people in their homes,
You will be called upon to give a lot of advice if your medical counterpart is not around.

Such as:

1. Nutritional advice. Understand that PLWHA's need a lot of extra nutrition and care. If they lose weight it is difficult to get it back. A daily Multivitamin is a good supplement. All of the other advertised supplements are mostly trying to make money. But if the problem is cancer, nutrition does not help as much. Just encourage whatever can be tasting good for the client.
2. Medicine advice. If the person is taking ARV's, never stop the drug without first consulting the doctor who prescribed it.
3. Pain advice. Know that medicines should be there for as long as the pain is there. For HIV/AIDS this is variable. But most cancer pain is constant and will not go away. Therefore the medicine also should not go away!
4. Social advice. You should understand all of the community resources available to your client. This will be a lot more than just what your facility is providing.
5. Wound advice. Are you prepared to change a dressing? Have your counterpart in nursing show you how it is done. Get confident. Know when to use gloves and carry some with you.
6. Hopeless situations. You will encounter people and places that seem hopeless. Use all of the elements of teamwork to bring hope and healing back into these circumstances. Be prepared ahead of time to encounter terrible difficulties. It is not every day but they are there.

18/02/2005

TAARIFA YA SIKU YA TATU

Vipindi vya siku ya tatu vilianza kwa sala iliyoongozwa na Mchungaji. Alisisitiza juu ya kazi hii kuwa ni ya kujitolea baada ya kujitambua kuwa kwa nini umekuwa mkristo na Mungu kwa nini amekuweka kwenye nafasi uliyonayo. Pia kama Yesu alivyowaita wanafunzi wake.

Baada ya hapo tulipata taarifa ya sikio kuhusu matukio mbalimbali huko Moshi, Dar, Tanga, Mbeya, New York na Baghdad – Iraq.

Baadaye ilifuatiwa na taarifa au ripoti ya day two baada ya ripoti hiyo kilianza kipindi cha kwanza ambacho kilikuwa ni group work. Kazi ya vikundi topic kila kituo kuandaa mipango ya kazi kwa muda wa miezi sita – kuanzia March hadi August namna ya kutatua matatizo.

Kazi hii iliendelea mpaka saa nne kamili na watu kutawanyika kwenda kupata chai. Baada ya kupata chai nzuri kabisa tuliendelea na kuwasilisha (presentation) mipango ya kazi kutoka katika vituo 17 vya washiriki zoezi hili liliendelea mpaka saa saba na nusu mchana na washiriki kuondoka kwenda kupata chakula cha mchana. Baada ya chakula cha mchana tuliendelea na kipindi cha pili chenye mada ya USHIRIKISHWAJI. Kazi hii ilifanyika kwa kikundi kisha kila kikundi kikawasilisha kila walichojadili kwa pamoja. Baadaye muhtasi wa ushirikishwaji ukatolewa na mwezeshaji.

Baada ya somo hilo kwisha mwezeshaji alimkaribisha Mkurugenzi wa Palliative Care Dr. Christopher Hartwig kutoa mpango mzima katika huduma hii kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za huduma za wagonjwa majumbani katika vituo vyetu akisisitiza juu ya mpango alitoa barua kwa kila kiongozi wa Kituo/Hospitali zilizotuma wajumbe kuhudhuria semina hii, na baada ya hapo Dr. Christopher mikakati yake jinsi ya kuboresha huduma hii kwa kueleza yafuatayo:-

1. Kuwatafutia elimu wanawarsha.
2. Pesa za kuendeshea semina nyingine.
3. Kuwa na mifuko inayojitegemea katika kila kituo kuhusu Palliative Care.
4. Kutafuta wageni/marafiki wengine wa Ospice kutoka mataifa mengine ya nje.
5. Kututafutia dawa Morphine iliyopatikana katika vituo vyetu.
6. Baada ya maelezo haya Mkurugenzi huyo alimkaribisha Mwenyekiti wa Semina Mch. Safari kushukuru kwa niaba ya wote. Kisha alimkaribisha Mchungaji Kimerei kufunga kwa sala. Alisoma neno kutoka Meth. 3:26-29. Mkazo tusiwe mbwa anaezuia ng'ombe kula majani asio kula yeye. Yaani usiwanyime watu yaliyo mema ambayo yapo katika uwezo wako.

Mwisho wanawarsha waliagana kwa sala ya Bwana.

DATA COLLECTION

1: Register Book:

- Client name, age, hospital number, diagnosis
- Date of entry to program, date of departure from program

2: Visit Record

- Who visited
- When visited
- Where visited (inpatient, home)
- How visited (on foot, bicycle, vehicle)
- Services provided: counseling/medicine/spiritual
- This can be done in a notebook for example one notebook for a year or a month

3. Patient Record

- A separate paper for each client, so that when they are seen multiple times, the services which you have provided are there for anyone to see
- Front of this paper: client particulars including initial list of problems. These problems include the physical, spiritual, psychological and even social/economic.
- Back of the paper: visit information each time the client is seen

4. Medicine Record

- Special record for which clients are on morphine, showing when medicine started, the dose, and when last visited
- Other special drugs for example free drugs from the government or other programs, which require a written notation of the medicine use.

5. Training: any activities you have done such as training volunteers in your community

These are the bare minimum of records which must be kept if your program is going to be taken very seriously from donors or at the national level.

One or two people, working in isolation with minimal outside support, do not need to keep many records. They each know everything. But if you are showing your work to an outsider, there must be clear records. There is no escape.

Reports should be submitted to your hospital leadership monthly. They should be simple, straightforward, and easily found in your day to day records. For example:

- Number of clients seen (home and in hospital)
- Total number of clients alive on program
- Number of AIDS cases and number of cancer cases
- Comment on amount of medicine used, for example number of clients on pain treatment; number of clients on special medicines for HIV/AIDS such as MVI or co-trimoxazole.

Home Based Care and HIV/AIDS

1. It is part of the 'continuum of care' given by the health facility

2. HBC supports clients, identifies clients, and cares for clients according to their level of need.

3. HBC is a center for referral to other helpful agencies in the community i.e. legal support, food support, hospital referrals according to the economic situation

4. Early identifying of Opportunistic Infections

5. Treatment of pain and other common medical problems i.e. nausea and vomiting, diarrhea

6. Having some basic drugs on hand:
   - Aspirin or Paracetomol
   - Multivitamins (supposedly all PLWHA's should take)
   - Co-trimoxazole (for all Stage 3 and 4 Disease)
   - Amitryptaline
   - ORS packets and/or advice

7. Able to give advice on ARV's if they are in your community. If they are not yet there, get good advice when the medicine arrives. Palliative Care and HBC are taught as part of the program for ARV use by the Tanzanian hospitals.

8. Building up PLWHA support groups, either in homes or at the hospitals or even the churches

9. Teamwork with an Emphasis on Spiritual Care